

KINA CHA FIKIRA



KAULI YA WALIBORA

"Leo nasema kwamba hakuna tija ya kufa sasa hasa kutokana na kizazi hiki cha watu makauleni wanaokusifu na kukukashifu kwa pumzi moja na kinywa kimoja."

HUU si wakati mzuri wa kufa. Hili halitokani na hatua alizopiga mwanadamu katika kuboresha miundumbini na teknolojia kwa jumla. Rafiki yangu mmoja, na sasa simkumbuki nani, aliniambia mwaka uliopita kwamba huu si wakati mwafaka kufa kwa vile ukifa unapitia na uhonda wa maendeleo ya mwanadamu katika uvumbuzi na ugunduzi wa mambo tumbi nzima. Sikubaliani naye hata sasa na sikukubaliana naye alipoyatamka aliyoyatamka. Nakubaliana naye kuhusu suala la kwamba sasa si wakati mwafaka wa kufa, ila kwa sababu yake sikubaliani naye.

Leo nasema kwamba hakuna tija ya kufa sasa hasa kutokana na kizazi hiki cha watu makauleni wanaokusifu na kukukashifu kwa pumzi moja na kinywa kimoja. Kifo cha aliyekuwa waziri mkuu wa kwanza mwanamke Margaret Thatcher 2013 ndicho kilichonindua kwa tabia hii ya kukirihisha. Watu walijificha nyuma ya pazia la majina bandia ya majukwaa ya mtandaoni kukomoa na kuua maiti. Walisema walivyojuka mwovu Bi Thatcher na kwamba dunia ilikuwa afadhali bila yeze. Nilimaka sana. Katika hukumu hakuna wakali kama watu wa kizazi kilichoko. Wanajua kuhukumu kuliko Mwenyeze Mungu, yaani machomipao. Hakimu wa haki kama wao hakuna. Wao ndio wajuo. Nani kama wao?

Nimeona tangu kifo cha rais wa kwanza wa Kenya, Mzee Daniel Toroitich arap Moi, mambo yamekuwa yale yale. Watu wanapozungumza hadharani kwenye runinga na mawanda rasmi, wanampalia sifa kiongozi huyo aliyetuacha mkono. Wakigeuka pahali ambapo si rasmi wanatembe cheche za matusi na lawama. Wanatukana tu na kutusi kama cherehani. Na hakuna pahali ambapo hilo limebainika zaidi kama katika majukwaa yaitwayo ya kijamii mtandaoni kama twitter, facebook and kwengineko.

Wanasema mabaya mpaka yanaku-

Kiswahili kilipata utanuzi mkubwa mno katika enzi ya Moi, makiwa kwa wote



chusha na kukuchosha. Mimi nishachoka.

Siwezi kufanya kazi ya Mwenyezi Mungu ya kuhukumu watu. Wacha wafao wafe, na hukumu tumwachie mwenyewe Muumba. Niliwahi kuhudhuri mazishi ya Profesa mmoja maarufu sana. Yeye alikuwa mijongoni mwa watu walionirai nipate kisomo cha tija.

Niliona vile waliopanda jukwaani walivyojsifu sana kwa umahiri wake wa kitaaluma na utu wake wema. Haya walikuwa wanayasema kwenye mikrofoni. Ila wakishuka toka jukwaani wanasesmezana wao wa wao kuhusu mapungukiwa au mapungufu ya marehemu. Mwone alivyokuwa hana mke, hana nyumba, kazikwa katika shamba la nduguye.

Hii ni nini hii? Wanamkosoa pakuba wa mtu ambaye hayupo hapa kujitetea mwenyewe dhidi ya lawama zao.

Katika siku hii ya mazishi ya Mzee Daniel Toroitich arap Moi, sina nia ya kumsifu wala kumkashifu, kama nikikopa maneno ya Bruto katika tamthilia ya Shakespeare cha Julius Caesar iliyoafisiriwa na Mwalimu Julius Nyerere. Nachotaka kusema ni kwamba ni katika enzi yake ambapo Kiswahili kilipata utanuzi mkubwa zaidi tangu kujipatia uhuru. Ni Mzee Moi ndiye aliyekifanya Kiswahili somo la lazima katika mfumo wa elimu.

Nasema makiwa sana kwa wote wanaohusika na msiba wa kuondokewa na Baba Moi.